


MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA MJINI MOSHI



MATUMIZI MABAYA YA MAJI

Baadhi ya Wateja wetu wana matumizi mabaya ya maji safi, tabia ambayo husababisha

- Ongezeko la Deni katika Ankara ya Maji ya Mteja ya kila mwezi na kulazimika kulilipa deni hilo ili kuendelea kupata huduma ya maji safi na salama,
- upotevu na hasara kubwa kwa rasilimali ya maji nchini mwetu na duniani kote, rasilimali ambayo ingeweza kutumiwa na wananchi wengine.

Ni jukumu la Wateja wa Huduma ya Maji Safi na Wakazi wa Mji wa Moshi kuhakikisha kuwa maji safi yanatumwiwa kwa uangalifu wa hali ya juu na kwa mahitaji muhimu tu. *Mambo yafuatayo ni baadhi ya tabia ambazo ni hatari. Jiepushe nazo!*





Usiache Bomba lako likidondosha maji kwa matone matone. Likibakia hivi kwa muda wa saa moja utakuwa umepoteza lita 4 (nne) na kwa massa kumi na mawili utakuwa umepotza lita 48 (arobaini na nane). Maji hayo itabidi kuyalipia kwa sababu ya kushindwa kufunga bomba yako vizuri.



Usisafishie vyombo kwenye bomba, matumizi ya maji huwa ni makubwa sana na itakubidi kulipia maji bila sababu

Usifulie nguo kwenye bomba, matumizi ya maji huwa ni makubwa sana na itakubidi kulipia maji hayo bila sababu



Unaposukutua meno yako usiache bomba lako linaendelea kutoa maji utalipia maji ambayo hukuyatumia

Mteja analazimika Kulipia Ankara ya Maji ambayo itatokana na uzembe wake wa kutodhibiti matumizi ya Maji katika nyumba ama eneo lake.

Kwa Maelezo zaidi ama Kuomba Ushauri Mteja atapaswa kuwasiliana na Kitengo cha Mahusiano na Wateja (Huduma kwa Wateja).

Jihadhari na Matumizi Mabaya ya Maji

**MKURUGENZI MTENDAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA
MJINI MOSHI**
S.L.P 324, MOSHI Simu: 2751164
Barua Pepe: muwasa@kilionline.com